**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SIMU YA UPEPO: "REGCOM "**
**SIMU NA:- 023-220-2098**
**FAX NA. 023-220-2502**
**Email: ras.lindi@pmoralg.go.tz**

**OFISI YA MKUU WA MKOA,**
**S.L.P. 1054,**
**LINDI.**

**13, Mei 201.9.**

# TARATIBU ZA USAJILI WA KAMPUNI ZA UNUNUZI WA ZAO LA UFUTA MSIMU 2019

Mkoa unawatangazia wanunuzi wote wa zao la ufuta kuwa, Msimu wa ununuzi wa zao la ufuta utaanza rasmi tarehe 25/05/2019. Mfumo wa ununuzi utakaotumika ni ukusanyaji wa ufuta kupitia vyama vya Ushirika vya msingi na kuuzwa kupitia minada itakanyofanyika kila siku ya jumamosi na jumapili ya wiki katika maeneo yanayolima zao hili.

Wanunuzi wote wanatakiwa kujisajili Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Lindi kabla ya kwenda kushiriki katika minada itakayofanyika. **(Hakuna kampuni itakayoruhusiwa kushiriki bila kusajiliwa).**

Mambo muhimu yatakayohitajika ili kampuni iweze kusajiliwa ni:-

i. Nakala ya leseni hai ya biashara (valid business license).
ii. Nakala ya cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN/VAT Certificate).
iii. Nakala ya hati ya kutodaiwa kodi ya ndani ya nchi (Tax clearance)
iv. Nakala ya cheti cha usajili wa kampuni (Certificate of incorporation/certificate of registration).
v. Picha mbili za rangi za wakurugenzi wa kampuni
vi. Taarifa za benki zisizopungua miezi mitatu (Bank statements).
vii. Baada ya kujisajili mnunuzi atapewa maelekezo ya namna ya kushiriki kulingana na mwongozo wa ununuzi wa ufuta uliyopitishwa na wadau wa ufuta mkoa wa Lindi.

**NB:**Utaratibu huu ndio utakaotumika msimu 2019 na usajili unaanza rasmi tarehe 13/05/2019.

Imeandaliwa na:-
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P 1054
**LINDI.**